

SILAHA NYENYE NGUVU: KUJISALIMISHA KWA BWANA

Zaburi 37:5, *“Mkabidhi Bwana njia zako, pia mtumaini, naye atafanya.”*

Tunajua kwamba mambo yote hutenda kazi kwaajili ya kutupatia mema kwa wale wampendao Yeye(Warumi 8:28). Ninajua ninaweza kumpenda yeye;Hilo ndio jambo pekee ninaweza kufanya (mathayo 22:36-40). Na ninasalimisha mambo yote kwake. Na kama kazi ni kubwa sana kwake,Ni nini maana ya kujaribu kwangu? Hakika. Yeye ndiye aliyelituma hilo, ni neno lake. Sitaki kuhubiri maneno yangu, Nataka nihubiri Neno lake. Sihitaji kuzungumza jambo Fulani kuhusu mimi binafsi, Nataka niseme jambo Fulani kumhusu yeye. Hivyo basi ni Neno lake, Nguvu zake.

Hiyo ndiyo sababu siamini kwamba mtu mmoja anaweza kumponya huyo mwingine. Hakuna jambo kama hilo katika maandiko.Lakini ninaamini kwamba Yesu Kristo mwana wa Mungu ameponya kila mtu mgonjwa ambaye alishawahi kuugua, kama wangelikubali hilo, na kuokoa kila mdhambi, kama tu wangelikubali hilo (Yohana 1:12-13; Zaburi 49:7). Lakini ni imani yako binafsi juu yake, kwamba umekubali na kuungama(kukiri) (Waebrania 4:14-16). [1]

Kama mtu Fulani amezungumza jambo kukuhusu, na wewe ukawajibu kwa kuwazungumza tena,Mungu hawezi kupigana pambano lako; Unapigana wewe binafsi(Kutoka 14:14). Hebu achilia hilo na umuache yeye afanye hilo. Na salimisha hilo tu kwake. Silaha kubwa sana niijuayo ya Mkristo leo, ni kujisalimisha kwa Mungu. Wakati huwezi kufanya lolote kuhusu hilo, hebu salimisha tu kwake, na Mungu atalishughulikia. Je hamuamini jambo hilo? [2]

Umeshawahi kuamka asubuhi na kusikia robin wote wakipiga kelele, ndege wote wadogo pindi tu kunapombazuka. Wakijipanga, na wakiinua vichwa vyao angani na kuimba, wakiimba, wakiimba. Huwezi sikia mmoja wao ana presha. Huwezi kuona mmoja wao mkongojo, Umewahi kuona? Mungu anawashughulikia (Mathayo 6:25-27). Hiyo ni kweli.Wao wanaamini hilo tu na kusalimisha kila kitu kwa Mungu, Na kuendelea mbele. [3]

Yesu alifanya nini? Aliweka macho yake kuelekea Kalvari. Yeye alikwenda moja kwa moja Yerusalemu kwa kutolewa kwaajili ya sadaka. Uzito wa kila dhambi ambayo imewahi kufanyika hapa duniani, au yoyote ambayo ingekuja kufanyika, ikawekwa juu ya mabega yake ya thamani (Yohana 1:29). Alikua mtu mkuu sana. Wakati watu wanapozungumza jambo Fulani baya kuhusu wewe, kama utaweza kuendelea mbele na kusahau hilo, hiyo inaonyesha ulivyo mkuu sana. Watu wadogo wahawezi kuvumilia hilo; Yeye alikua mkuu sana kuweza kusikia wakimkosoa. Alikua na jambo moja la kufanya; nalo lilikua mapenzi ya Baba (Yohana 5:30); 6:38). Yeye alipaswa kufa kwaajili ya watu wote (Mathayo 20:28; Yohana 10:17-18).

Hivyo akaendelea mbele huku uso wake ukielekea Kalvari. Unaweza kuwazia, Uzito ndani yake, kuangali kule, Gesthemane (Mathayo 26:36-46), yale maumivu ya Golgotha (Mathayo 27:33-53), Kukataliwa kwa Mungu, Dunia ikawa giza, mabega yake yakisugua, uso wake ukitoka damu, Majeraha yake. Yote yalikua juu yake, hata kilio chake “Baba, ikiwezekana, kwamba kikombe hiki...” Na yeye-Uchungu wa namna ile mpaka Maji na Damu yake vikatengana na kudondoka kutoka ubavuni mwake. Hakuna kitu, isipokua uchungu mkali sana ndio ungeweza kufanya hivyo. Yote yaliwekwa juu yake (Luka 22:39-46). [4]

“Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikua juu yake; na kwa kupigwa kwake sisi tumepona” (Isaya 53:5). Kila kitu kiko wakati uliopita. Hakuna mtazamo hasi kabisa katika Ukristo; Yote yako sawa, Imekwisha kupiwa. Imemalizika (Yohana 19:30) Amina. Wazia kuhusu hilo. Yote imekwisha, imemalizika. Mungu hangefanya la ziada tena; Yote yamekwisha. Kristo amesimama hapa usiku wa leo, Ungeweza kusema, “ Bwana Yesu Kristo niponye” Yeye angesema, “ Nimeshalifanya hilo.” Ungesema, “Niokoe Bwana Yesu” ‘Nimekwisha kulifanya.” Wakati alipokufa Kalvari, kila dhambi iliyowahi kufanyika au ama ingekuja kufanyika, ilisamehewa pale kwa damu iliyomwagika. Lakini haitafanya lolote na wewe mpaka uwe umeikubali hiyo. Inapaswa iwe mali yako binafsi, na hiyo ni Imani yako binafsi kwa kazi iliyokwishamalizika, ambayo kristo amefanya kwaajili yako (Waefeso 2:10). [5]

Daktari anasema huwezi kupona, lakini Mungu anasema ninaweza. Hivyo nitalichukua kwa njia hiyo na hivyo ndivyo nitakavyoliamini. Ndio bwana. “ Oh jamani, bado ninajisikia kuumwa kama nilivyokua jana usiku.” Haitaleti tofauti yoyote. Hebu kua muamini imara, kua wa kimiujiza zaidi kwaajili ya kesho kupata hilo. Amina. Huo ni uzao wa Ibrahimu. Usiyumbe kwenye ahadi za Mungu (Warumi 4:20-21).

Daktari angefanya yote awezayo, hayo ni yote angeweza kufanya. Lakini Mungu hajafanya yote awezayo. Jambo lolote lililo kubwa kwa Mungu, siwezi kupambana nalo. Hivyo ninalisalimisha hilo kwake na kuendelea mbele. [6]

Wakati Fulani uliopita,wakati nlipookolewa, Nililiweka hilo kichwani pangu kama hivi;Sitakwenda kuogopa chochote ambacho Mungu amesema, Kwasababu Mungu anaweza kutunza Neno lake Mwenyewe, na Jambo lolote ambalo ni kubwa sana kwa Mungukufanya, iko wap sababu ya mimi kuhofu kuhusu hilo? Amina (Wafilipi 4:6-7).

Kama yeye ni Mungu mwenyezi,Anaweza mambo yote. Kama hawezi ufanya mambo yote, basi yeye sio Mungu mwezi. Hivyo ninamuamini yeye kua Mungu mwenyezi.Hivyo ninajisalimisha mimi mwenyewe kwake, Nafsi yangu, mwili wangu, Uhai wangu, pumzi yangu,kufa kwangu,ufufuo wangu, vyote kwake, na siku moja tukufu, Yeye atakuja (Zaburi 62:1-2,5-8; Waebrania9:27-28). [7]

Sasa, unapofukia mbegu,ninyi wakulima, unachukua na kwenda nje hapana kupanda mbegu zako, huendi kila siku asubuhi na kuifua,na kusema, “hebu nione sasa, Je inakua? Chochote kimetokea kwayo? Hapana.” Unarudisha hiyo chini.siku inayofuata, unasema, “Nataka kuona kama inaendelea vizuri” unafukua hiyo tena; Haitakua kwa namnahiyo.Vema, ambounalofanyana mbegu, unaisalimisha kwenye ardhi,unaifunika; hivyo ndivyo ungeweza kufanya kuhusu hilo. Ni juu ya Mungu kufanya yote yaliyobakia.

Vema,Hivyo ndivyo ilivyo kwa Neno la Mungu. Kama utachukua ahadi yoyote ya kiungu Mungu aliyoahidi kwenye Bibli yake, iweke moyoni mwako, na imwagilie kila siku kwa kumtukua Mungu(Zaburi34:1), na hiyo itakuja kutendeka, itakua, kamautaacha kufanya mzaha na hiyo, kama utaiacha hiyo yenyewe. Usiseme, “Hebu nione, ninaweza kucheza kidole changu leo, Je ninajisia vizuri kidogo, Je maumivu ya kichwa changu yamepungua kidogo?” oh, hapana, haiwezi kua hivyo kamwe, salimisha hilo tu kwa Mungu, na kaa mbali nalo, na uliache hilo. Hiyo ni mbegu ya Mungu. Itakua(Marko 4:26-28). [8]

Hapa ndipo udhaifu wa hao wanaojiita wakristo wanaposhindwa kupokea uponyaji wao (ahadi zao)leo. Wanaangalia ule uvimbe badala ya kile Mungu alichosema. Unaweza kuwazia kuhusu mkulima akipanda mbegu zake na kwenda kila siku kufukua yote, kuona kama yanaenda kuota au laa? Hatapata mazao kamwe. Anaisalimisha hiyo kwenye udongo, kuhusu hilo Mungu ameahidi na hiyo humaliza hilo.

Hivyo ndivyo tunavyopokea kila neno la Mungu, sababu ni mbegu na tunaipokea hiyo mioyoni mwetu(Warumi 10:10) hebu isalimishe hiyo kwa Mungu na usahau kuhusu hiyo. Mungu atafanya yote yaliyobakia maana aliahidi atatenda. Neno la Mungu. Na kila neno litazaa kile lilicho, Kwamaana Neno ni Mbegu (Luka 8:11). [9]

Ahadi yoyote ambayo Mungu anaahidi,wewe ipande tu moyoni mwako na useme “ Ni yangu, Mungu amenipa hiyo” Sasa, unaweza usione matokeo yoyote sasa. Huwezi kuona mche wa mhindi punde tu unapopanda mbegu yako, ila kwa hakika uko pale. Kwavile utaiacha pale, na kuendelea

kuimwagilia, itakua. Usihofu kuhusu hilo. Kama ni mbegu yenye uoto..... Na kila Neno la Mungu huotoshwa na Mungu mwenyewe. Mungu yuko ndani ya Neno, Hivyo litakua. Mnajua litakua

Hapo mlipo. Tunapaswa kuchukua Neno lake, kulikubali, kuliadini hilo, lisalimishe hilo, Na hilo litakua. Hiyo ni sawa. Usiendeleo kuifukua hiyo sasa. Utaiharibu hiyo. Utaharibu mazao yako kila wakati unapofanya hilo. Kwahiyo salimisha tu Kwa Mungu na Uliadini hilo. [10]

Lakini mara zote hatujui, unajua; Mungu hutenda kazi kwa namna ya siri kufanya maajabu yake. Kama tukisalimisha chochote kwa Mungu na kuadini, kama tu watoto wetu ama chchote kile, hebu na tuadini kwamba Mungu atajibu yale maombi (matendo 16:30-31). Hebu salimisha tu hilo kwa Mungu. Hiyo ni yote upaswayo kufanya. Na usiweke mkono wako juu ya hilo tena. Muachilie Mungu hilo. Kama utaenda kufanya jambo Fulani kuhusu hilo, basi Mungu atasimama nyuma na kukuacha uendeleo nalo mpaka umalize. Lakini unapolisalimisha kwa Mungu na kumuachia yeye, basi yeye atalifanya. Wewe mwadini tu. Simama nyuma tu, na usitende chochote, ila amini. Hapo ndipo neema huhesabiwa kwa wenye haki, kama utaliadini hilo Mungu atafanya (Warumi 4:5). [11]

Nisikilizeni. Ninakwenda kusema jambo Fulani kuu. Kila mara unapoangalia dalili zako, unachelewesha uponyaji wako. Usiifukue hiyo tena. Imesalimishwa kwake ambaye ameahidi kuponya, Yeye ambaye amewaponya wengine (Hesabu 21:4-9).

Unapopita katika mstari wa maombi na mikono ikawekwa juu yako, Biblia inasema, “Maombi ya imani yatamponya mgonjwa” (Yakobo 5:15). Usiseme, “Vema, hebu nione kama ninajisikia vizuri kidogo, moyo wangu vizuri kidogo, mikono yangu....” Usifanye hivyo. Unalichelewesha hilo. Lisalimishe kwenye udongo kwasababu ni mbegu. [12]

Aidha itachipua, chochote itakachofanya, usijali. Mungu ameahidi hilo, na kwa hakika unao uponyaji wako unapokubali huo. Upo katika namna ya Mbegu (Isaya 53:4-5). [13]

Tunajaribu kufanya Mungu kama tarishi, “Bwana, Wewe nifanyie *hili*! Na Wewe nifanyie *hili*! Na Wewe nenda ufanye *lile*,” kumwambia Yeye jambo la kufanya.

Yesu alisema, “Mwombapo, ombeni hivi, ‘Baba Yetu Uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe. Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike.’” Ambaye, unaona mahali tunafanya hilo? Daima tunamtaka Mungu kutufanyia kazi zetu, ama kutufanyia jambo fulani. Lakini tukiwa tayari kusema, “Mapenzi Yako yafanyike,” (mathayo 6:9-10). Nani ameona amabapo tunafanya hilo? Mara zote tunataka Mungu afanye utumishi kwaajili yetu, au kufanya jambo Fulani kwaajili yetu. Lakini tunapotamani kusema, “Mapenzi yako yatimizwe” kujikabidhi Kwake, kuzikabidhi njia zetu Kwake. Yote tuliyo, tuyakabidhi Kwake. Hapo ndipo Mungu atakaposogea, wakati ukiwa tayari kumruhusu Yeye afanye kazi juu yako, si wewe kufanya kazi juu Yake. [14]

Wakristo hapa, kuna wengi wa Walutheri wakiketi hapa, Wabaptisti, msiwalaumu hao watu, wanaishi katika wakati wao. Yesu alisema, “kila neno la Mungu ni mbegu” Je hiyo ni sawa? Mpanzi alitoka kwenda panda Mbegu. Yeye alisema, “mimi, Mwana wa Adamu, ninapanda mbegu na Mbegu ni Neno la Mungu” (Luka 8:11) Na kila wakati unapoona hili Neno linasema chochote, ni

mbegu. Na tunapandwa kwa Mbegu ya Mungu isiyoharibika (I Petro 1:23) Na kama mtu atachukua Ahadi ya Mungu yoyote ya Kiungu moyoni mwake na kuimwagilia na imani, itazaa kilekile tu ilichosema itafanya.Amina. Usijali ni nini. Chukua tu Ahadi ya Mungu ndani ya moyo wako.... [15]

Neno lote alilonena Mungu, halina budi kutimizwa. Mungu hawezi kusema lolote bila kulifanya litimie. Akiisha kulinena, ni kazi iliyomalizika(Warumi 4:13-21). Imekwisha tayari wakati Mungu anapolinena. Mungu kamwe haneni mpaka Yeye awe tayari kwa ajili ya hilo kutimia; na, anaponena, ni kama tu limetimia tayari.

Sasa, kama hilo halitatupatia msingi wa kuiweka imani yetu asubuhi ya leo! Mungu anaponena Neno, limekwisha tayari. Na vipi kuhusu ahadi Zake ambazo Yeye ametupatia? Kila kitu ambacho amesema, ni kazi iliyokwisha tayari(Mwanzo 1:3-4). Kwa hiyo, basi, tunapolipokea Neno Lake moyoni mwetu, tayari limetimia, limekwisha! [16]

Ni Roho Mtakatifu, leo, akiwinda mioyo miaminifu ambayo itaamini Ujumbe huo. Kila kitu katika Biblia, kilichoahidiwa, ni kwa ajili ya mwaminio huyo. Na wakati unapolikubali hilo katika utimilifu wake, na Mungu anajua ya kwamba utafanya jambo hilo, Yeye anakupa hatimiliki hakiki ya jambo hilo(Waefeso 1:13-14). Ndipo basi kila ahadi iliyoahidiwa ni mali yako, na Roho Mtakatifu yupo hapo apate kuihuisha hiyo kwako(Warumi 8:11-17). [17]

Basi vipi unaweza kusema unaweza kua mkristo mzuri ukikaa nyumbani kama tu vile ungekua kanisani? Huwezi kufanya hilo. Soma Neno! Roho Mtakatifu anakula Neno. Biblia ni mlo wa kiroho wa Mungu kwaajili ya kanisa lake. Na Roho Mtakatifu ndiye anayelileta kwako na kuliweka moyoni, na kwa shukrani unalimwagilizia hilo. Na kila Ahadi ya Kiungu itazaa kilekile ambacho Mungu alisema ingefanya. Itafanya. Ni Neno lake, na ni Uzima wake (Yohana 6:63-64). [18]

Tunafahamu Roho Mtakatifu anakula Neno. Na hebu Roho Mtakatifu wa Mungu achukue Neno na kuupa kila moyo, kwakadiri tu tulivyo na uhitaji nalo. [19]

Oh, Ndugu, unaweza usijue ni kitu cha namna gani, unapojishusha chini na kijisalimisha kabisa kwa Mungu. Usitumie akili yako mwenyewe. Usitumie fikira zako mwenyewe (Mithali 3:5-6). Salimisha tu njia zako kwake na utembe jinsi atakavyokuongoza (Zaburi 37:5).

Kama atakwenda njia hii, hiyo yote ni sawa. Wakati mwingine inaongoza kuelekea maji yenye kina kirefu, lakini mnajua wimbo unaosema: “Baadhi hupitia kwenye maji, baadhi hupitia mafurio, Baadhi hupitia majaribu mazito, lakini wote hupitia kwenye Damu.” Njia ya Mungu ikiongoza kupitia bahari yenye kina kirefu, katika jangwa, na juu ya milima, kwenye Jangwa la dhambi, na mengineyo. Lakini Mungu atakutoa, kama utamfuata yeye na sio kujaribu kutumia mawazo yako mwenyewe. Fanya tu kile Mungu amesema ufanye, na utakua salama. Mnaamini hilo? [20]

Mungu anaweza kutumia kila kipaji cha utu wetu kama ukikabidhi...ukisalimishwa Kwake. Anaweza kutumia nia yetu, ndoto zetu, dhamira yetu ya ndani, dhamira yetu ya kwanza, ulimi wetu, nyimbo zetu, macho yetu...Kila kitu tulicho nacho kinaweza kutumiwa na Mungu kikikabidhiwa kwa Mungu. Unaona? Kila kitu ulicho, kikabidhi kwa Mungu. Yeye atatumia kila njia na kila sehemu yako, Yeye ataitumia. Haijalishi ni nini, Yeye ataitumia iwapo imetakaswa kwa kusudi Lake na wito. [21]

Ninamjua niliye muamini. Ninasadiki kwamba anaweza kulinda ambacho kimesalimishwa. Kama Mungu amesema lolote, Mungu hutunza Neno lake. Na yeye ni Yule jana leo na hata milele (Waebrania 13:8). Na nitaendelea kurikodi kwanjia ya kanda na kadhalika kama hivyo, lakini ninasema hili, kwamba mtazamo sahihi juu ya Ahadi yoyote ya kiungu ya Mungu, utalifanya itimie. Kumbuka kwamba. Kama utachukua Mtazamo sahihi juu ya hiyo, Ahadi, Utalifanya itimie. Hebu Mungu ajaalie hilo. [22]

Ndugu Branham akiongea katika Maombi:

Ninajikabidhi sasa Mungu. Ninakabidhi njia zangu, mawazo yangu yote, yote nifanyayo. Hebu nisiwazie tena fikira zangu. Hebu nisiwe tena na njia yoyote ya kilimwengu. Hebu vyote vikatakaswe. Hebu nikawe msafi tu, Mawazo matakaifu kuanzia leo na kuendelea. Hebu maisha yangu yote yakawe yake.

Zungumza kupitia kwangu, Bwana. Sitasema fanya hili mpaka uwe umeniagiza hilo. Umeagiza Injili yako ihubiriwe na mwanadamu. Ungeweza kuagiza upepo kuhubiri hiyo. Ungeweza kuagiza nyota kuhubiri hiyo. Ungeweza kuagiza mwezi, jua, kuhubiri hiyo. Ila umemuagiza mwanadamu. Hutabadili hilo. Unasubiri mtu. Husubirii nyota, hivyo vinakutii wewe. Upepo ungekutii. Lakini Bwana, sisi wanadamu, hatuna jema; Hatukutii wewe. Bwana, Utusamehe, Je utatusamehe? Utatusamehe sisi? [23]

Ee Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, Mtoaji wa vipawa vyote vilivyo vema, Ninafuata Huu muongozo, kwasabu nimefundishwa kwamba Mwanao ameshinda masumbuko yangu yote. Ninamkubali yeye kama mshindi wangu. Na ninakabidhi yote yaliyo yangu kwake, nikiamini kwamba Magonjwa yangu, au chochote kinisumbuacho kitaniacha. [24]

Tusaidie Bwana. Ninaomba kwaajili ya kila mtu Bwana. Ninaomba maombi ya imani kwaajili yao wote. Sasa, Kwa wote ambao wamefungua mioyo kwaajili ya Neno la Mungu, kwa imani ninapanda hii mbegu. Ninadai hao kwa Jina la Yesu Kristo na kwa imani katika Mungu, Kwamba, Bwana Mungu, Ninawasalimisha kwako sasa. Nyweshea mbegu (Isaya 44:3); tuma Roho juu yake, Bwana, ile mbegu inayochipua pale, kwamba wewe ni Mungu yuleyule Mkuu kuiponya, Mungu yuleyule mkuu kuokoa, Mungu yuleyuke mkuu wa ufufuo. Wewe ni Mungu. Hebu wakazae mazao, Bibi-arusi kwaajili ya Bwana wetu Yesu, Tumbo la moyo lililotakaswa kwaajili ya kupokea Neno. Jalia hilo Bwana. Ninasalimishakwako uchukue kuanzia hapa, kama ikiwezekana, kila mmoja wa Bibi arusi wako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina [25]

Nukuu:

[1] “Mkombozi, Ukombozi” (55-1119), Aya 50

[2] “Hadithi ya maisha” (51-0722A), Aya 9

[3] “Ufufuo” (53-1205), Aya 55

[4] “Batimayo kipofu” (56-0414), Aya 31

- [5] “ Msilizeni yeye” (56-1215) aya 11
- [6] “ Agano lisilo na Masharti” (54-0306) aya 164-165
- [7] “ Nguvu ya shetani” (55-1005) aya 47-48
- [8] “ Tuonyoshe Baba na itatutosha” (62-0731) aya E44
- [9] “ Uhai ndio huponya” (57-0611), aya 38-39
- [10] “Mabwana, tunaweza kumuona Yesu” (62-0724), aya E54
- [11] “ Mwana wa Daudi, unirehemu” (61-0215), aya E16
- [12] “ Tuonyeshe Baba itatutosha” (62-0722) aya E51
- [13] “ Kesi ya mahakamani” (64-0412) aya 88
- [14] “Ulimwengu unaporomoka tena” (63-1127), aya 77-78
- [15] “ Nitarejesha kwenu, asema Bwana” (54-0809A), aya E35
- [16] “ Imetupasa kutimiza haki yote” (61-1001M) aya 83-84
- [17] “ Muhuri ya pasaka” (65-0410) aya 118
- [18] “ Kuzika” (57-0420) aya 54
- [19] “ Mzabibu wa kweli na divai ya uongo”(55-0607) aya E9
- [20] “ Kwa Neno” (53-1204) aya E48
- [21] “ Vipawa vya Mungu hutafuta mahali pake” (63-1222) aya 41
- [22] “ Yesu Kristo yeye Yule jana leo na hata milele”(58- 0207) aya E58
- [23] “Ushawishi” (63-0112) aya 303-304
- [24] “ Mshindi mkuu” (58-0110) aya E60
- [25] “Lile Neno lililonenwa ndio mbegu ya asili” (62-0318), Aya 462-463

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

*Joseph C Kanju
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: kanjujoseph23@gmail.com
Cellphone: 0654335361*